

Nani anapaswa kupimwa? Naweza kupimwa?

Mtu yeyote anayetimiza vigezo vilivyoainishwa hapo chini anaweza kupimwa kwa ajili ya COVID-19:

- Mtu yeyote mwenye na dalili za COVID-19
- Wafanyakazi wa afya
- Mtu yeyote wa umri zaidi ya miaka 60
- Mtu yeyote ambaye ana magonjwa fulani
- Wanakaya walio katika mazingira magumu ambayo yametajwa hapo juu
- Wafanyakazi wa utunzaji wa watoto
- Wafanyakazi ambao hawawezi kuzuia kutangamana na wenzao au umma kwa ujumla
- Mtu yeyote asiyeonyesha dalili zozote

Ninawezaje kupimwa?

Unaweza kupimwa kwa:

- Kupigia simu mtoa huduma wako wa afya
- Kupigia simu ConvenientMD 1-833-263-0131
- Kwa kusajili kupitia [fomu yetu ya usajili kwa upimaji](#) [testing registration form] au kupigia simu kwenye 603-271-5980
- Kupigia simu Idara ya Afya ya Mji wa Nashua [Nashua City Health Department] kwenye 603-589-3456 kama unaishi au unatumika katika mji huo.
- Kwa wakazi wanaoishi katika eneo la Greater Manchester, tafadharo pigia simu Manchester COVID-19 Hotline kwenye 603-668-1547 ili kuchunguza chaguo za kupimwa katika eneo lako.

Ni nini kipimo cha vipambana vya mwili [antibody]? Naweza kupata kipimo cha damu cha vipambana vya mwili vya COVID-19?

Kipimo cha vipambana vya mwili huchunguza Sampuli ya damu ya mtu kutafuta vipambana vya mwili vya SARS-CoV-2, virusi vinavyosababisha COVID-19. Vipambana vya mwili hivi vinazaliwa wakati mtu ameambukizwa, kwa hiyo matokeo chanya ya kipimo hiki yanaonyesha kwamba mtu alikuwa na uwezekano wa awali kuambukizwa na virusi. Vipimo vya vipambana vya mwili hupatikana sasa kwa njia ya maabara ya kibiashara kwa ajili ya kugundua vipambana vya mwili dhidi SARS-CoV-2. Vipimo vya vipigana vya mwili havipaswi kutumiwa kwa kutambua uambukizi kali wa COVID-19 kwa sababu inaweza kuchukua wiki 2 baada ya maambukizi ili vipimo vya vipambana vya mwili viwe chanya. Haijajulikana bado kama mtu mwenye kipimo chanya kwa vipambana vya mwili huwa na kinga kwa ajili ya uambukizi wa SARS-CoV-2 au ana uwezekano wa kuwaambukiza wengine. Watu ambao wanapimwa chanya kwa vipambana vya mwili vya COVID-19 wataitwa na Idara ya Afya ya Umma.

Je, inawezekana kupimwa mapema mno katika mwendo wa ugonjwa?

Katika awamu za mapema za maambukizi, inawezekana virusi visitagunduliwe na vipimo vya virusi.

Nilisikia ni vigumu kupata kipimo. Je, hiyo ni kweli?

Hiyo ilikuwa kweli wakati wa mwanzo wa janga hili, lakini vipimo vimepanuliwa kwa mtu yeyote katika NH ambaye anataka kupimwa.

Nikasikia kuna Kitengo Jongevu cha kupima COVID-19. Ninawezaje kujisajili?

Mfumo wa Kukabiliana na Matibabu wa Mji Mkuu [Metropolitan Medical Response System] (MMRS) nikitengo binafsi cha wafanyakazi wa kujitolea, kinachotoa vipimo jorgevu kuchagua vikundi katika jimbo.

Nilipimwa na niliambiwa ningeweza kupata matokeo kutoka Maabara ya Umma ya NH afya ya umma maabara (NH PHL). Ninawezaje kupata matokeo yangu?

Kama ulipimwa kupitia mtoa huduma wako wa matibabu, huduma za haraka, au hospitali, mtoa huduma ambaye alitenda kipimochako atakupata na matokeo ya kipimo chako cha COVID-19. NH PHL na DPHS wanaweza tu kutoa matokeo ya kipimo cha COVID-19 kwa mhudumu wa afya ambaye aliamuru kipimo.

Wote maabara ya kibiashara na Maabara ya Umma ya NH (NH PHL) wataripoti matokeo ya vipimo kwa wahudumu ambao waliamuru vipimo hivyo.

Ni wakati gani wa kurejea kwa matokeo ya vipimo vyangu kutoka Maabara ya Umma ya NH (NH PHL)?

Wakati wa kurejea si *chini* ya saa 72 kutoka wakati NH PHL inapata sampuli [specimen] yako. Hiyo inamaanisha kama ulipimwa siku ya Jumatatu, sampuli yako inaweza kuwa bado haijafika kwenye NH PHL hadi Jumanne. Matokeo yako hayatakuwepo hadi Ijumaa (maabara ya kibiashara yanaripoti wakati sawa wa kurejea).

Ni nani ninaweza kumwita ili kupata matokeo ya kipimo changu?

Ni muhimu kukumbuka kwamba utakuwa tu unawasiliana na mtoa huduma ambaye aliamuru kipimo chako. Maabara ya NH PHL na ya kibiashara wataripoti tu matokeo kwa mhudumu aliyeamuru kipimo, na *hawataoa matokeo ohayo kwako ikiwa unawaita moja kwa moja.*